Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Enyi mlioamini! Tubuni kwa Allah toba iliyotakasika; huenda Mola wenu Akawafutieni maovu yenu na kuwaingizeni katika Pepo zipitazo mito chini yao, siku ambayo Allah Hatamfedhehesha Mtume na wale walioamini pamoja naye;... Surah 66:9

JUZU 80 No. 218 | SAFAR-RAB.I 1442AH | OKT-NOV 2020 | TABOOK 1399 HS | BEI TSH. 500/=

Maisha ya Mtume Mtukufu Muhammad saw

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

Yalivyosimuliwa na Hadhrat Mirza Bashir ud Din Mahmud Ahmad r.a. Khalifatul Masih wa pili

KUZALIWA KWA MTUME MUHAMMAD S.A.W.

Mtume Muhammad s.a.w. alizaliwa ndani ya mazingira haya. Baba yake aliyeitwa Abdullah alifaraiki kabla hata ya kuzaliwa kwake. Babu yake mzaa baba, Abdul Muttwalib, aliwachukua yeye na mama yake, Hadhrat Amina katika hifadhi yake.

Sawa na desturi za Kiarabu, yeye alikabidhiwa kunyonyeshwa kwa mwanamke Fulani (Bi Halima) aliyeishi maeneo ya jirani na Taif. Waarabu walikuwa wakiwakabidhi watoto wao kwa wanawake wa vijijini ili lugha yao iwe iliyotakasika na afya yao iwe njema.

Ndani ya mwaka wake mmoja (baada ya kutoka kwenye malezi ya Bi Halima, alipokuwa na umri wa miaka sita), mama yake alifariki njiani kati ya Makka na Madina alipokuwa akirejea akitokea Madina alikokwenda kuwatembelea wazazi wake na alizikiwa hapo hapo. Na kijakazi Fulani akamleta Muhammad



s.a.w. Makka na kumkabidhi kwa babu yake mzaa baba.

Alikuwa na miaka minane wakati babu yake huyo naye pia akafariki na baba yake mdogo, Abu Twalib, akawa muangalizi wake sawa na wasia wa baba yake (Abdul Muttwalib).

Alipata fursa mbili au tatu za kwenda nje ya Bara Arabu ambapo moja kati ya safari hizo ni wakati alipokuwa na umri wa miaka 12 aliposafiri na baba yake mdogo, Abu Twaalib, aliyekuwa amekwenda Sham (Syria) kwa ajili ya biashara. Safari yake hii, ilikuwa imeishia tu katika miji ya kibiashara ya kusini mashariki mwa Syria. Kwa sababu hakuna popote yalipotajwa maeneo kama ya Baitul Muqaddas n.k. katika safari hii. Baada ya hapo, aliendelea kubakia Makka hadi alipofikia umri wa ujana.

KUSHIRIKI KWAKE KATIKA JUMUIYA YA HILFUL FUDHUUL

Tabia yake tangu utotoni ilikuwa imeelekea kwenye kuwazia na kuyatafakari mambo na alikuwa hajiingizi kwenye magomvi ya watu, bali alikuwa akishiriki katika kuondoa fujo na kupatanisha magomvi. Hivyo baada ya kuchoshwa na mapigano ya mara kwa mara kati ya watu wa Makka na makabila ya vijiji vya pembezoni mwake, wakati baadhi ya vijana wa Makka walipoanzisha jumuiya Fulani iliyokuwa na makusudio haya kwamba wao watakuwa wakiwasaidia wenye kudhulumiwa, basi Mtume s.a.w. akajiunga kwa shauku kubwa ndani ya Jumuiya hiyo. Wanachama wa Jumuiya hiyo walikula kiapo kwa maneno haya kwamba:

"Wao watawasaidia waliodhulumiwa na kuwapatia haki yao maadam tone moja la bahari litaendelea kuwepo na

Endelea uk. 5

Kwa nini Biblia Ni Jibu Wanamkana Nabii Issa kuwa Si Yesu?

Na **Juma Iddy Abeid**
Kigoma

Kundi maarufu linalo jiita biblia ni jibu.Limekuwa liki jaribu kupotosha umma wa waumini wa wa kristo kuwa Issa na Yesu ni watu wawili tofauti.Ni kundi hilo peke yake hapa Tanzania ndio linalo weka wasiwasi katika mioyo ya watu wasio wachunguzi .Maana wapo waandishi wengi wa kristo waliofanya uchunguzi wakaona hakuna tofauti ya Issa na Yesu.

Mfano kipo kitabu kiitwacho Hisory of the Arabs, cha Philip .K. Hitt, Kitabu hicho kwa umuhimu wake. Kimenukuliwa ndani ya kitabu kiitwacho JITIHADA YA AINA YA BINADAM YA KUMTAFUTA MUNGU. Ukurasa 285 Ameandika karibu masimulizi yote ya kihistoria ya Quran yanaulinganiwayo wa Kibiblia kuanzia kwa Adam, Nuhu, Ibrahim (wanatajwa karibu mara sabini katika sura ya ishirini na tano katika sura tofauti tofauti Najina la mmoja wapo likiwa kichwa cha sura ya 14) Yani sura IBRAHIM

Akiendelea anasema: Miongoni mwa watu wa AGANO JIPYA yupo zakaria , Yohana mbatizaji Yesu (Issa)n Mariyamu ndoo pekee wana kaziwa kwa uchunguzi wakulinganisha.Huo ni mfano mmoja tu wa wasomi wa ulaya .Waliofanya utafiti wakimaandishi .Waapo wengi ndio maana nikasema hilo kundi la biblia nijibu linapotosha waumini wao. Katika kalatasi lao walilo lichapisha nakuliuzashilingi elfu mmoja .lenye kichwa cha habari : JE NABII ISSA <A.S> NDIE YESU KIRISTO ?: Katika ukurasa wa kwanza wanadai kuwa wameangalia kwa makini yani kwa undani zaidi hoja ya Issa na Yesu kuwa ni mmoja au watu wa willi walio tofauti wakaangalia vipengele tisa;

1: Majina na maana zake za asili yake, yaani maana ya jina Issa na maana ya jina Yesu .

2: Kuunbwa kwa Issa je Yesu akuunbwa?

4: Je Manabii waliwawatabiri?

5: Nassaba (wazazi)

6: Mamlaka

7: Hukumu

8: Kufa kwao

9: Kurudi kwao

Tatizo hawa kutoa vigezo vyao kama ni vya kisheri na kihistoria au kimazingira nani na hisi ni mbinu tu ya kutaka mafanikio ya kuwaburuza waumini motoni kuwa bwana Yesu alisema kipofu akimuongoza kipofu wote

Endelea uk. 4

Muujiza wa Masihi Mauúd uk. 10

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

KILA UGONJWA NA DAWA

Hivi karibuni Rais wa Ufaransa ametoa madai kuwa Islam imo katika hatari. Ni madai mazito na ni jambo la busara kuuliza, Nani yumo hatarini, Ufaransa au Islam. Historia itatusaidia kujibu swali hili.

Mwaka 1789 kulitokea mapinduzi nchini Ufaransa. Mapinduzi hayo yalijengeka kwenye misingi ya Uhuru, Umoja na Usawa. Kumbe madai hayo yaliuwa kwa watu fulani. Waliobaki kwa mathalani Afrika tukavamiwa na Wafaransa wakati wakauwa, nyumba zikachomwa na utamaduni wetu ukabezwa na kudharauliwa. Huko Algeria chini ya Ben Bella ilipiganwa vita ya muda mrefu na damu nyingi ya Algeria ilimwagika. Hatujui ni kwa kiasi gani mlikuwa mnakumbuka vile mnavyofikiri kuwa mnavithamini, Uhuru! Umoja! Usawa! Mara baada ya uhuru wa bendera mmeendelea kuyaua yaliyokuwa makoloni yenu kwa kutumia kanuni hizo mnaziheshimu na kuzienzi.

Kwa hivi sasa Ufaransa mmebanwa na ugonjwa wa Korona. Tatizo la Ufaransa sio Islam. Tatizo la Ufaransa ni utamaduni wa kuwa ndumilakuwili. Huku mnasema hivi na kule mnatenda vile. Damu za hao mliwateketeza lazima zitaendelea kuwasuta na kuwasumbua. Sheria hizo mnazianzisha lengo lake ni kufuta utamaduni hamtafanikiwa. Islam ni Kaaba ya Allah. Jeshi lolote litakalotakakuvamiatunawakumbusha yaliyowapata watu wa tembo.

Nasi Waislam wakati umefika wa kuungana na kuwa na sauti moja. Kuunganisha Islam na kuwa na sauti moja lazima itoke kwa mjumbe aliyetumwa na Allah. Mjumbe huyo amekwishafika. Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. Udhaifu wa Islam unatokana na kutokuwa chini ya nidhamu aliyoanzisha. Dawa ya matatizo yetu ni kukiuka kuta hizo na kuingia nyumbani kwa Masihi Aliyeahidiwa.

Tangazo la Tanzia

Assalam alaikum warahmatullah wabarakatuhu!

Tunasikitika kuwaarifu ndugu wote wanamakundi ya mtandaoni katika majina yake mengi kwamba mwenendo mwema wa kimaadili ya ubinadamu na uislam umetutoka – **innalillah wa inna ilaihi rajiun.**

Hatukubahatika kufikwa na mauti haya kwa ghafla jambo ambalo huenda lingeweza kuwa jema kwa kuwa alama yetu ibakiayo juu ya ardhi ingekuwa hafifu na ya kufutika mapema. Kinyumeche kifo hiki kilianza zamani kwa namna ya pole pole na kisirisiri huku kikiongezeka kwa kina, ukubwa wa mkumbo wake na upana wa athari zake.

Tungejuaje kwamba utonaji wa kifundi wa maneno changamshi ulofanywa mara nyingi na wasomi wetu tuwajuao na tuwapendao sana, ulikuwa uje kuzua wimbi la kauli na misemo isiyopitishwa kwenye mizani ya utu wala kupakwa hata tone la mbali la mtizamo wa lengo letu la msingi na la daima – **Islam kwanza**, mpaka ikajakuwa upayukaji ndio mtindo wetu mpya tulio wengi, na ndio unaotupendeza zaidi kuuandika na kuusoma na tunaufurahia zaidi kadri unavyoongezeka kuwa wa hovyo na unaohasiri heshima za watu binafsi na hata maslahi mapana ya **Jamaat Ahmadiya**, Inayosimamia **Mapenzi kwa wote bila Chuki kwa yeyote.**

Bundi mdogo alilia sana katika zama za kati za mchakato wa kifo hiki lakini hakusikilizwa labda kwa sababu sauti yake haikuwa kubwa pale tulipoanza kudiriki kurushiana kejeli, kudhalilishana, na kutunishiana misuli katika makundi yetu na tukafanikiwa mno katika hili kiasi wengi wa wanaojistahi wakajiondoa makundini na wengi wa waonao haya ya kiutu wamebaki kuduwaa kimya wakitutizama kwa kutumaini kwamba labda yatapitamo mambo yenye kufaa ingawa inahitajia subra kubwa kuyatafuta yaliyo **halisi** kwenye maziwa yenye matone ya usaha.

Bundi mkubwa alishaanza kulia siku nyingi katika zama hizi pale tulipoongeza ujasiri wetu katika '**kupakana**' kwa kile tunachokiita kuambiana ukweli. Maana hatukutosheka na kupakana matope bali tukaamua ili kuonyesha msisitizo tupakane **mavi yetu wenyewe.** Ole wetu, Bundi huyu mkubwa ni mzoefu mno, halii mpaka mabadiliko katika afya ya jumla na hali ya viungo nyeti anavyovijua katika elimu yake ya siri iwe imefikia pahala ambapo tukio lenye kuleta majonzi limewadia kweli.



Maombolezo yetu yanaweza kuwa na maana na kutuletea nusra ikiwa yatakuwa ya dhati na tutajiuliza kati ya mengine mengi; Ni kweli hatuwezi kuwaelekeza watu kwenye wema kwa njia ya wema?, Ni kweli ni lazima katika kusema kwetu kweli tutumie lugha zisizo staha na hata matusi?, Ni kweli hatuwezi kuiga mfano bora wa lugha za kuongelea uliopo katika maandiko sufufu ya Jamaat Ahmadiyya?, Sisi hasa ni nani, tunatoka wapi na tunakwenda wapi na tutafika tuendako kwa mwenendo huu?.

Dua yetu ya kimya hatimae inabidi iwe kwamba tunakuomba Mola wetu utuepushe na dua iliyomo kwenye kirihiko la wote tunaowakirihi kwa **ujuha wetu huu wa kisasa**, na hasa wale tunaowatukana lalamiko lao lisipokelewe kwako ewe mola wetu kwa kuwa **tumeelemewa na kulewa na nguvu na mvuto wa mtandao**, na onyo lililoko kwenye wimbo huu wa moyo wa mshairi muungwana Sheikh Shaaban Robert libaki kuwa kweli ila sisi lisituguse hata kidogo pale aliposema:

Aombewae laana, dua zikizidi sana, wokovu huwa hana, bali ni kuangamia!

Tunakuomba Mola wetu kwa ajili yetu sisi uliotujaalia kuzaliwa au kujiunga na silsila adhimu ya Masih (as) wa Mtume wako Mteule (saw) utuongoze tuutumie mtandao na makundi yetu kugawana **hazina za kiroho** tulizozipata kwa kufanya **juhudi zinazokubaliwa mbele yako**, na utuokoe na kamato hili la shetani linalotupeleka tusikokwenda na tukishindwa yote basi angalau sote tuimbe kama ndugu yetu anayetajwa kwa haki, Sheikh Kaluta Amri Abeid pale aliposema; **nisije kuteremka, ngazi ipandishayo – Amin.**

Limetolewa na mtazamaji wa pembeni ya uwanja

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Pongezi kwa kukamilisha ahadi za Tahrik-e-Jadid 2019 - 2020

Amir na Mbashiri Mkuu, Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry sahib anayo furaha kutoa pongezi kwa viongozi na wanajamaat wote wa mikoa ifuatayo, ambao wamefaulu kwa kukamilisha makusanyo ya Tahrik-e-Jadid kwa mwaka 2019 - 2020

Pia anaiasa mikoa ile ambayo imeshindwa kukamilisha makusanyo sawa na ahadi zao, wajitahidi kukamilisha ingawa mwaka umeisha, kwani ahadi ni deni sawa na mafundisho ya Qur'an Tukufu.

Aidha, ni matumaini yake kuwa mwendo huu utaendelezwa kwenye makusanyo ya Waqf-e-Jadid. InshaAllah.

1. Mwl. Abdullatif Ngarombe Sahib - Mkoa wa Simiyu
Nafasi ya kwanza kitaifa katika kukamilisha Bajeti na kuvuka lengo kwa asilimia 140.

2. Mwl. Ramadhan Mahmood Sahib - Mkoa wa Geita
Nafasi ya pili kitaifa katika kukamilisha Bajeti na kuvuka lengo kwa asilimia 138.

3. Sheikh Khurram Shahzad Sahib - Mkoa wa Ruvuma
Nafasi ya tatu kitaifa katika kukamilisha Bajeti na kuvuka lengo kwa asilimia 135. Pia umekuwa nafasi ya Nane kitaifa kwa kukusanya kiasi kikubwa.

4. Sheikh Shafi Muhammad Memon Sahib - Mkoa wa Arusha
Nafasi ya nne kitaifa katika kukamilisha Bajeti na kuvuka lengo kwa asilimia 134. Pia umekuwa nafasi ya saba kitaifa kwa kukusanya kiasi kikubwa.

5. Sheikh Abid Mahmood Bhatti Sahib - Jamia Ahmadiyya Kihonda
Nafasi ya tano kitaifa katika kukamilisha Bajeti na kuvuka lengo kwa asilimia 126.

6. Sheikh Asif Mahmood Butt Sahib - Mkoa wa Morogoro
Nafasi ya sita kitaifa katika kukamilisha Bajeti na kuvuka lengo kwa asilimia 123. Pia umekuwa nafasi ya tatu kitaifa kwa kukusanya kiasi kikubwa.

7. Sheikh Imrani Mahmood Sahib- Mkoa wa Shinyanga
Nafasi ya saba kitaifa katika kukamilisha Bajeti na kuvuka lengo kwa asilimia 120. Pia umekuwa nafasi ya tisa kitaifa kwa kukusanya kiasi kikubwa.

8. Sheikh Khawaja Muzaffar Sahib- Mkoa wa Dodoma
Nafasi ya nane kitaifa katika kukamilisha Bajeti na kuvuka lengo kwa asilimia 109. Pia umekuwa nafasi ya sita kitaifa kwa kukusanya kiasi kikubwa.

9. Sheikh Abdulwahid Sahib - Mkoa wa Tabora
Nafasi ya tisa kitaifa katika kukamilisha Bajeti na kuvuka lengo kwa asilimia 105. Pia umekuwa nafasi ya kumi kitaifa kwa kukusanya kiasi kikubwa.

10. Sheikh Karimuddin Shams Sahib - Mkoa wa Mbeya
Nafasi ya kumi kitaifa katika kukamilisha Bajeti na kuvuka lengo kwa asilimia 104.

11. Sheikh Muhammad Afzal Bhatti Sahib - Mkoa wa Tanga
Nafasi ya kumi na moja kitaifa katika kukamilisha Bajeti na kuvuka lengo kwa asilimia 104.

12. Sheikh Riaz Ahmad Dogar Sahib - Mkoa wa Iringa
Nafasi ya kumi na mbili kitaifa katika kukamilisha Bajeti na kuvuka lengo kwa asilimia 101. Pia umekuwa nafasi ya tano kitaifa kwa kukusanya kiasi kikubwa.

13. Sheikh Nadeem Ahmad Sahib - Mkoa wa Dar es Salaam
Nafasi ya kumi na tatu kitaifa katika kukamilisha Bajeti na kuvuka lengo kwa asilimia 101. Pia umekuwa nafasi ya kwanza kitaifa kwa kukusanya kiasi kikubwa.

14. Sheikh Mussa Issa Sahib - Mikoa ya Mtwara & Lindi
Ham kukamilisha Bajeti yenu kwa asilimia 100% lakini nina wapongezeni kwa kushika nafasi ya Pili kitaifa kwa kukusanya kiasi kikubwa.

Chumvi na Afya Zetu

Na **Mtaalamu Wetu**

Chumvi hutumiwa kila siku na wanadamu katika vyakula, lakini pale inapotumika kwa



wingi inaweza kuleta madhara ya kiafya.

Chumvi inapokosekana katika baadhi ya vyakula huvifanya kukosa ladha nzuri hivyo ni vigumu kuacha matumizi ya chumvi.

Uwepo wa kiambata cha sodium katika chumvi ndiyo sababu ya wataalamu wa afya kuonya juu ya matumizi makubwa ya chumvi, hii ni kutokana kuongeza msukumo wa damu mwili.

Msukumo unapokuwa juu kupita kiasi ni kihatarishi cha kuweza kupata matatizo ya moyo na kiharusi (stroke).

Magonjwa haya mawili ndiyo chanzo cha vifo vingi katika nchi zenye uchumi wa kati mpaka mkubwa.

Vilevile ulaji wa chumvi nyingi unahusishwa na kutokea kwa magonjwa mengine ikiwa saratani ya mfuko wa chakula, udhaifu wa mifupa, unene na mawe katika figo.

Taasis kubwa za afya duniani ikiwamo Shirika la Afya Duniani (WHO) zimekuwa zikitoa mapendekezo mbalimbali ya kiasi cha chumvi ambacho ni salama kiafya kutumia kwa siku.

Kiujumla duniani kote kiwango cha chumvi ambacho ni salama kinachopendekezwa kutumia kwa siku ni miligramu 1,500 ambacho ni karibia na nusu kijiko cha chai na isizidi miligramu 2,300.

Tafiti zinaonyesha kuwa kiwango hiki cha chumvi ni salama kwa matumizi na hakiambatani na upandaji mkubwa wa msukumo wa damu mwilini.

Inakadiriwa kiwango cha ulaji chumvi kwa watu waliowengi kwa siku ni miligramu 2,300-3,400 kwa siku ambacho ni sawa na kijiko kimoja cha chai mpaka na kimoja na nusu kwa siku.

Kiwango hichi ni hatari kiafya, ni vizuri kuchukua tahadhari mapema na kuanza kujidhibiti kutumia kiasi kikubwa cha chumvi hasa chumvi ya kuongeza mezani.

Kwa mazingira yetu ya Kitanzania, chumvi huliwa zaidi hasa wakati wa kula nyama choma, chipsi na vyakula vya migahawani au katika sherehe.

Katika mazingira haya watu wengi hutumia zaidi chumvi ya mezani na kuiongeza kiholela katika mlo wanaokula.

Ni ngumu zaidi kukadiria kiasi cha chumvi kilicho salama kwa kutumia kichupa chenye tundu.

Mbinu ambayo ni rahisi ambayo



inaweza kusaidia kupunguza utumiaji chumvi usio salama hasa ya mezani ni ile ya kuchukua chumvi kwa mtindo wa kufinya na dole gumba na kidole cha shahada.

Kiasi ulichofinya katika vidole hivyo ndiyo unatakiwa kula kwa mlo huo.

Kumbuka kinga ni bora kuliko tiba, kudhibiti ulaji wa chumvi nyingi ni rahisi kuliko madhara yake ambayo ni vigumu kuyatibu yanajitokeza.

Chukua tahadhari mapema! Tumia chumvi kwa kiasi.

Kwa nini Biblia Ni Jibu Wanamkana Nabii Issa kuwa Si Yesu?

Kutoka uk. 1

wataingia motoni:

BIBLIA KISHERIA INA YESU ZAIDI YA MMOJA

Wanaanzia hapo kujiuliza ,Ikiwa Yesu wapo wawilli au zaidi watakuwa wana mlenga yupi sie Issa na yupi ni Issa pia kama hao Mayesu walio ndani ya biblia watatofautiana vipi Quran ilaumiwe ?Kwakuwa Biblia ina Yesu wawili kisheria . Hakuwa lazima mmoja pia awe na mashaka na Mwingine pia huwenda mmoja hatakuwa ndie Issa . Zaidi ya hapo kutakuwa na hila kuficha kweli .Nakuomba ndugu msommaji twende pamoja katika uchunguzi ili atakapo toa hukumu uone ushaidi ulivyo vurugwa ili kumkimbia Issa hebu nianze kuonyesha vigezo vyao waalivyo tumia kama hoja kumkana Issa.

1:NASABA :Wamedai ili mtu kumtambua ana toka na nani huanzia kwa wazazi kisheria ,Huwezi kuanzia kwajina tu hilo nikweri. Lakini pia kisheria ni majina matatu pia yaani jina la mhusika jina la Baba na jina la Babu.Mdaiwa wa ndani ya Qurani ameita ISSA BUN MARIYAM kwa maana mtu asiye julikana utababani au hana baba .huyo ndio kundi la biblia ni jibu wamemkataa hawezu kuwa ndiye Yesu wanaye mjua wao.

Kutokana na hilo kuna tofauti kubwa mno katiya Yesu aliye tajwa na vitabu vine vya injili .Injili mbili hazikuandika wazazi hivyo .wale ambao hawakuwaandika wazazi hawana nafasi yakutoa ushahidi wa kumkataa ISSA BUN MARIAM kuwa sio Yesu.

Sasa hebu tuwafuate hao walio wataja wazazi kina saba kama walivyo daiwa na kundi hilo la biblia ni jibu.Moja ya Injili ni Injili ya Mathayo 1-16 kitabu cha ukoo wa Yesu kristo ukoo wa Daudi,Mwana wa Ibrahim, alimzaa Isaka ,Isaka alimzaa Yakobo akamzaa Yuda na ndugu zake .Yuda akamzaa Peresi na Zera kwa Tamari Peresi akamzaa Esrom aka mzaa Aramu ,Aramu akamzaa Amina dabu akamzaa Nashoni ,Nashoni akamzaa Solomoni ,Solomoni akamzaa Boazi kwa rahabu Boazi aka mzaa Obedi kwa Ruthu ,Obedi akamzaa Yese ,Yese akamzaa Mfalme Daudi na Daudi akamzaa Selemani kwa yule mke wa uriya .Selemani akamzaa Robohani akamzaa Abiya akamzaa Assa. Tukianza Mathayo 1-12-16: Na baada ya ule uhamisho wa babeli Yekonia akamzaa Sheatieli ,Sheateli akamzaa Zerubabeli akamzaa Eliudi akamzaa Eliudi akamzaa Eliazeri Matani akamzaa Yakobo akamzaa Yusuf Mumeise Mariam alie mzaa Yesu aitwa kristo.

YESU MWENYE UKOO MWINGINE

LUKA 3:23-38 Na Yesu Mwenyewe alipoanza kufundisha akidhaniwa kuwa ni mwana wa Yusufu wa Eli wa Mathati wa Laisi wa Melk wa Yona wa Yusufu Matathia wa semeo, wa Yusufu wa Yuda wa Yohana wa Rosa wa Zerubabeli wa Shealti wa Neri wa Melk wa Abi wa Kosani wa Elidani wa Eli wa yosua wa yoram wa Mathati wa Lawi wa Semeri wa Yuda wa Yusufu wa Yonani wa Eliakum wa Melea wa Mena wa Matatha wa Nathani wa Daudi wa Yese wa Obedi wa Boazi wa Selmani Wa Nashoni wa Aminadabu wa Aramu wa Hesron wa Peresi wa Yuda wa Yakobo wa Isaka wa Ibrahim wa Tera wa Nahori wa Sarugi wa reqan wa pelegi wa Ebari wa Sela wa Kanani wa Enosh wa Enosh wa Sethi wa Adam wa Mungu

Ebu chunguza kwa makini muandiko wa Mathayo ambayo yalikusanywa huko Palestine (karibu 41w.k wakati uliyo usishwa 2k.w.k 33w.k nay ale ya mtakatifu Luka ambae anadai alifanya utafiti wakina sawa na Luka 1:1-4 ambae alikuwa kaiseria ambae alikamilisha uandikaji karibu 56-58 w.k

Hapo ukitulia utaona wazi wa Maandiko kwani Luka anasema Yesu alitokana na Yusufu wa ELLI wa Mathatti wa Lawi na Mtakatifu Mathayo yeye alimfahamu Yesu Bin Yusufu Bini Yakobo Bin Matani:Kanuni ya ki sharia huwa ni Ubin wa BABA NA BABU hivyon walimu wa biblia ni jibu wawa eleze wanafunzi wao Yesu yupi ambae sie Issa katika izo tofauti za Mayesu hao wawili wa Luka na Mathayo? Hivyo kabla ya kuelezea kwenye hoja ya majina na maana zake kwanza endelea kuwafahamisha wasomaji wa kikristo kuwa wapo Mayesu wawili Hivyo tuendelee tuone maisha ya utotoni mwao

YESU WA MATHAYO:

MATHAYO :2:13-14 Baada yawale wageni kuondoka Malaika wa Lisana alimtokea Yusufu katika ndoto aka mwambia amka umchukue mototo na mama yake mkimbilie Misri .Hivyo Yusufu aliamka akamchukua mototo pamoja na mama yake akaondoka usiku akaenda Misri .Baada ya hapo anadaiwa kuwa Herode alitua amri kuhuwa watoto wote .Mthayo 2:15:Herode alipo gundua kuwa Maajusi wamemdanganya alikasirika saana akaamuru watoto wote wakiume wauwawe waliopo Bathelehamu na kandokandom yake wenye cnini ya umri wa miaka miwili na chini yake .

Kurejeshwa kwake kutoka Misri : MATHAYO 2:19: Baada ya kifo ch Herode Malaika wa bwana limtokea Yusufu katika ndoto kule Misri akamwambia tena amka umchukue mototo pamoja na mama yake urudi katika nchi ya Israeli maana walio taka kumuua mototo uyo wa meisha kufa .

Hapa pana onesha yesu BIN YUSUFU BIN YAKOBO BIN MATANI alitoroshwa nakurujeshwa upya baada yakifo cha maadui zake lakini huyu Yesu mwingine wa Luka yeye ni mwingine na hakutoroshwa wala kurejeshwa Ni mwingine sababu yeye ni YESU BIN YUSUFU BIN ElliMathati BIN LAWI

LUKA 2:4-6 Yusufu na aliondoka Galilaya toka mji wa nazareti kapanda kwenda uyahudi mpaka mji wa Daudi,uitwao Bethelehamu kwakuwa yeye nimbari na jamaa ya Daudi ili andike pamoja na Marizim mkwewe ambae ame mposa ana mimba

Ikawa katika kukaa huko siku zake za kuzaa zikatimia . Akamzaa mwanae kwa kujifungua mimba akamvika nguo za kitoto akamlaza katika holi la kulia n"gombe kwa sababu hawakupata na fasi katika nyumba za wageni.

LUKA 2:21: Siku nane baada ya wakati wa kumtahiri mtoto ulipo fika walimpa jina Yesu. Jina ambalo alikuwa amepewa na malaika na malaika kabla hajachukuwa mimba .

N

HUYU YESU YUSUFU BIN ELLI BIN MATHATTI BINI LAWI. Anaonekana safari yake yakwanza ni luka 2:22:Siku zilipo timia za Yusufu na Mariam kama ilivyo Torati ya Musa,walikwenda nae toka Yerusalem wamuweke kwa bwana kila mtoto alie kifungua mimba ya mamae na aitwe mtakatifu kwa bwana

KURUDI VAZARETI

LUKA 2:39-40: Basi walipokwisha kuyatimiza yote kama hili vyo agizwa katika sharia ya bwana walirejea galilaya mpaka mjini kwao Nazareti yule mtoto akakuwa akaongezeka nguvu imejaa hekima na neema ya Mungu ilikuwa juu yake mpaka hapo hakuna tukio la kukimbizwa Misri kama Yesu Yusufu Bin yakobo Bin Matani alie toroshewa nchini Misri

SAFARI YA PILI

LUKA 2:41- Basi wazee wake huenda Yerusselem kila mwaka wakati wa sikukuu na alipo pata umri wake miaka kumi na miwili walipanda kama ilivyo desturi ya sikukuu lilipo kwisha kutimiza siku wakati wakurudi kwao yule mtoto Yesu alibika nyuma huko Yerussalemu.

MAONGEZI YA UTOTONI

LUKA 2:52 Nae Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo. Akimpendeza Mungu na wanadamu kama inavyonesha huyu Yesu hakutoroshwa katika utoto ni mwake kinyume na yule alie kimbinzwa Misri .Vipi wasiwe ma Yesu wawili tofauti vipi sasa waanze kumkataa ISSA BUN MARIYAM ndani ya Quran kuwa sio Yesu .Je ni Yesu yupi huyo?ni yule Mathayo au wa Luka ?isije kuwa mmoja ndie Issa na mwingine akawa ndie wenu ambae hawezi kuwa ndie Yesu.

Ambae hawezi kuwa Issa huyo utamjua mbeleni kwa vigezo na atakae kuwa Issa a.s pia tutamjua kwa mafundisho yao.Kabla ya uchambuzi huo ngoja tuendelee kuangalia wanafunzi .Je maYesu hao mawili walikuwa wanafunzi ?nakama walikuwa nao je majina yao yalitajwa? Nianze na Yesu alie toroshwa wakati wa utotoni nakurudishwa baada ya mbaya wake kufariki kama tulivyo ona kwanza kuzaliwa yeye hakujulikana ni wapi alizaliwa .Haikutajwa kama ni kisimani au zizini au mtendeni .Wala haijalishi kama hali hesabiwa katika sensa au la maana walimkimbiza usiku kwa usiku ili asi uwawe.Huyu wanafunzi wake ni kumi na mbili Mathayo 10:2 Yakobo wa Zebedayo na yohana nduguyu filipo na Bathomayo na Tomasi na Matayo mtoza ushuru.yakobo na Thadayo,simoni Mkananayo na Yuda Iskariyoti ndie msaliti hayo ndiyo majina ya wanafunzi wa Yesu alie pelekwa uhamishoni.

Hebu tuone majina ya wanafunzi wa Yesu ambaye yeye hakutoroshwa ambae waliishi hapo hapo na wazazi wake hadi akakuwa nakupata wanafunzi.

LUKA 6:13-16: Hata kulipo kuwa mchana aliwaita wanafunzi wake akachagua kumi na wawili,Miongoni nwanao aitwe.

Endelea uk. 11

Maisha ya Mtume Muhammad s.a.w



Kutoka uk. 1

kama hawataweza kufanya hivyo basi wao watawalipia haki zao wale waliodhulumiwa.”

Huenda fursa ya kukitekeleza kiapo hiki haikupatikana kwa yeyote mwingine minghairi yake. Wakati alipotoa madai ya unabii na Kiongozi wa Makka, Abu Jahal, akawa aliyehusika zaidi kuliko wote katika kumpinga na kuanza kuwaambia watu kwamba; Msiseme chochote na Muhammad, msiliamini neno lake lolote, mumdhalilishe kwa kila njia iwezekanayo, wakati huo mtu Fulani aliyekuwa amemkopesha Abu Jahal alikuja Makka na kumuomba Abu Jahal amlipe deni lake. Abu Jahal akakataa kumlipa deni lake. Mtu Yule akawashitakia jambo hili baadhi ya watu wa Makka na baadhi ya vijana, kwa utukutu tu, wakamuelekeza kwa Mtume s.a.w. wakimwambia kwamba aende kwake naye atamsaidia. Matarajio yao yalikuwa hivi kwamba aidha yeye atakataa kumsaidia, kwa kuzingatia upinzani ule uliokuwa ukifanywa dhidi yake kwa ujumla na watu wa Makka na hasa uliokuwa ukifanywa na Abu Jahal, na kwa namna hii angedhalilika mbele ya waarabu na kusemwa kuwa ni mvunjaji wa kiapo, au angekubali kumsaidia na kwenda kwa Abu Jahal na hivyo angemdhalilisha kwa kumfukuza nyumbani kwake.

Mtu Yule alipokwenda kwa Mtume s.a.w. na kumshitakia juu ya Abu Jahal, basi yeye, bila ya kusita, akainuka na kwenda naye na alipofika mlangoni kwa Abu Jahal, akapiga hodi. Abu Jahal alitoka nje na kumuona Yule mdai wake akiwa amesimama pembeni ya Mtume s.a.w. Mtume s.a.w. mara moja akamuelekeza kwamba wewe unadaiwa na mtu huyu kiasi kadhaa, hivyo mlipe. Na Abu Jahal akamlipa haki yake bila hata kuguna.

Wakati viongozi wengine wa Makka walipomlaumu Abu Jahal kwamba wewe ulikuwa ukituagiza tumdhalilishe Muhammad s.a.w. na tusihusiane naye kwa chochote, lakini wewe mwenyewe umelitii agizo lake na kumpatia heshima. Basi Abu Jahal akasema; Kwa haki ya Mwenyezi Mungu, kama ninyi pia mngekuwa mahali pangu, basi mngefanya hivi hivi. Mimi niliwaona ngamia waliokuwa wamelewa wamesimama upande wa kulia na wa kushoto wa Muhammad s.a.w. waliokuwa wakitaka kuniangamiza kwa kunikaba koo. Ni Allah tu ndiye ajuaye vema kama kuna ukweli wowote katika riwaya hii au la. Je ni kweli Allah Alionyesha ishara fulani au alielemewa tu na hofu ya ukweli? baada ya kuona hivi kwamba Yule mtu ambaye anayekejeliwa na kuchukiwa na watu wote wa Makka amepata ujasiri wa kusimama mbele ya mlango wa kiongozi wa Makka na kumwambia kwamba mlipe mtu huyu haki yake unayostahili kumlipa, hivyo haiba ya ukweli ikaivunjavunja roho yake ya utukutu naye akalazimika kukiinamisha kichwa chake mbele ya ukweli.

NDOA YA MTUME S.A.W. KWA BI KHADIJA R.A.

Muhammad s.a.w. alipokuwa na umri wa miaka 25 basi umaarufu wa wema na ucha Mungu wake ulikuwa umeshaenea mjini. Watu walikuwa wakimnyooshea kidole na kusema huyo mtu mkweli anapita. Huyo mtu mwaminifu anapita. Habari hizi zikamfikia pia mjane Fulani tajiri wa Makka naye akamuaomba baba mdogo wa Mtume s.a.w, Abu Twalib, kwamba amwambie mwana wa nduguye, yaani Muhammad s.a.w. kwamba asimamie mali za biashara yake zinazoelekea Syria na msafara wa biashara. Abu Twalib alimuewleza jambo hili naye akaliafiki.

Alifanikiwa mno katika safari hii na akarejea na faida kubwa kuliko iliyotegemewa. Khadija r.a. akahisi kwamba faida hii haikutokana tu na hali ya soko, bali ilitokana na wema na ucha Mungu wa kiongozi wa msafara. Akamuuliza mtumwa wake aliyeitwa Maisra, ambaye alikuwa pamoja na Mtume s.a.w., juu ya hali ya Mtume s.a.w. Naye pia akunga mkono wazo lake Bi Khadija na akasema kwamba uaminifu na ubora alioutumia safarini unaweza kutekelezwa na yeye pekee. Jambo hili likamuathiri mno Hadhrat Khadija r.a. Juu ya kwamba wakati huo, yeye, (Bi. Khadija r.a.) alikuwa na umri wa miaka arobaini na alishakuwa ameolewa katika nyumba mbili, akamtuma rafiki yake Fulani kwa Mtume s.a.w. ili afahamu kwamba je atakuwa radhi kumuoa (Bi Khadija)? Rafiki Yule wa Bi Khadija akamuendea (Mtume s.a.w) na kumuuliza kwamba: ‘Kwa nini wewe hauoi?’ Mtume s.a.w. akamjibu kwamba: ‘Mimi sina mali yoyote iniwezeshayo kuoa.’ Mwanamke Yule akasema: ‘Kama tatizo hili liondoke, halafu mwanamke Fulani mwema na mwenye mali atake kuolewa nawe! Akauliza: ‘Ni nani huyo mwanamke?’ Akajibu; ‘ni Khadija.’ Akasema nawezaje kumfikia!?! Hapo mwanamke Yule akasema: ‘Niachie mimi.’ Akajibu nimekubali.

Ndipo Hadhrat Khadija r.a. akatimiza adhma yake ya kuolewa kwa baba mdogo wa Mtume s.a.w. na akamuoa Hadhrat Khadija r.a. huu ulikuwa mlango wa kwanza wa utajiri uliofunguka kwa kijana aliyekuwa masikini na yatima. Lakini jinsi alivyoutumia utajiri huu, lilikuwa ni tukio lenye somo kwa ajili ya dunia nzima.

KUWAACHIA HURU WATUMWA NA HABARI ZA ZAID

Baada ya ndoa yake, wakati Hadhrat Khadija r.a. alipohisi kwamba, hisia za moyo za Mtume s.a.w. hazitapata ladha yoyote kwa maisha ya aina hii, kwamba mkewe awe tajiri na yeye anakuwa ni mwenye kumtegemea, basi akamwambia Mtume s.a.w. kwamba; ‘mimi nataka kukupa mali zangu na watumwa wangu.’ Mtume s.a.w. akauliza: ‘Ni kweli ewe Khadija?’ Alipokiri mara ya pili Mtume s.a.w. akamwambia; ‘Kazi yangu ya kwanza itakuwa ni mimi kuwaachia huru watumwa.’

Kwa hiyo wakati huo huo akawaita watumwa wa Bi Khadija na kuwaambia: ‘Ninyi wote kuanzia leo mko huru.’ Na sehemu kubwa ya mali akaigawa kwa masikini. Miongoni mwa watumwa aliowaachia huru, alikuwemo mmoja aliyeitwa Zaid. Yeye alikuwa ni mjanja na mwenye akili zaidi kuliko watumwa wengine. Kwa sababu yeye alikuwa ni kijana aliyetokana na ukoo uliotukuka na kuheshimika, ambaye aliibwa na majambazi wakati akiwa motto mdogo naye akaendelea kuuzwa (utumwani) hadi akafika Makka.

Kijana huyo, kutokana na ujanja na akili zake, akafahamu kwamba utumwa chini ya mtu huyu ni bora zaidi kuliko uungwana. Hivyo wakati Mtume s.a.w. alipowaachia huru watumwa akiwemo pia na Zaid, basi Zaid akasema: ‘Wewe waniachia huru lakini mimi sipendi kuwa huru, mimi nataka kuishi tu na wewe.’ Kwa hiyo akawa anaishi naye na siku hadi siku, upendo wake (kwa Mtume s.a.w.) ukawa unaongezeka.

Kwa kuwa yeye alikuwa ni kijana aliyetokana na ukoo tajiri, basi baba yake mzazi na baba yake mdogo walikuwa wakiwafuatilia majambazi wakimtafuta mtoto wao. Hatimae wakafahamu kuwa motto wao yuko Makka. Kwa hiyo wakaja Makka na baada ya kufahamu wakafika kwa Mtume s.a.w. na kumwambia: ‘Tafadhali mwachie huru mtoto wetu na uchukue kiasi chochote cha fedha upendacho. (Mtume s.a.w.) akasema: ‘Mimi mbona nimeshamuachia huru Zaid? Yeye anaweza kwenda nanyi kwa furaha kabisa.’ Kisha akamwita Zaid na kumkutanisha na baba yake na baba yake mdogo.

Pande zote mbili zilipokutana na kuifuta simanzi ya mioyo yao kwa machozi, basi baba ya Zaidi akamwambia (mwanawe) kwamba; ‘Mtu huyu mwema amekuachia huru, mama yako hana raha kwa kukukumbuka, hivyo tafadhali haraka uende kwake ili uwe sababu ya raha na utulivu kwa ajili yake.’

Zaid akasema; ‘Ni nani asiyekuwa na upendo kwa mama aua baba yake? Hata moyo wangu pia haujakosa upendo huu, lakini upendo wa Muhammad s.a.w. umeishapenya ndani ya moyo wangu kiasi hiki kwamba mimi siwezi asilan kutengana naye. Nimefurahi kukutana nanyi lakini kufarakana na Muhammad s.a.w. kuko nje ya uwezo wangu. Baba yake Zaidi na Baba yake mdogo walimsihi sana lakini Zaid hakukubali kwenda nao.

Baada ya kuuona upendo huu wa Zaid, Mtume Muhammad s.a.w. alisimama na kusema: ‘Tangu mwanzo Zaid alishakuwa huru, lakini kuanzia leo yeye ni mwanangu.’ Baada ya kuiona sura ya hali hii, baba na baba mdogo wa Zaid wakarejea nchini kwao na Zaidi akabakia Makka milele.

Bustani ya Washairi

YAKINI

Kikombe kimetakata, kwa nje kinavutia
Kwa kila anayepita, mate anakimezea
"Na mimi ningekipata, fuadi ingetulia"
kumbe siri ya maiti, aijuae muosha!

Pamwe na mshika kata, maji anayemwagia
Kimya huwa aina sita, lolote kujisemea
Kila mpenda kubwata, kichwani zimepungua
Akatula omungoma, kamanywa omubambi

Uzuri wenye kumeta, ni ndani kuchungulia
Yaliyomo ni mafuta, au uchafu ajaa
Bila yakini tajuta, katika hino dunia
Tizama nje na ndani, kuupata utulivu

Kaditama hujapata, bileshi wajisumbua
Yakubidi kujikita, kiini kukifikia
Au utaula mwata, janga utajivunia
Na kila mvuna janga, hula pamoja na wake

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)
Kiwalani, Migombani, Dar es salaam

WOKOVU

1.Salamu Ndugu zanguni, kwa mola naegemea,
Alhamdu rahmani, nuru kwa kunangazia,
Nimezaliwa kundini, Ahmad memjua,
Vitabuvye darasani, Mengi akanifumbua,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

2.kuwekwa msalabani, na damu wakamtoa,
Si wokovu tambueni, mungu alishakataa,
Ismaili jangwani, mola alimkataa,
Kwa wahayi Wa ndotoni, kondoo akamtoa,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

3.kabla kufika mbeleni, akili yako tumia,
Wema Wa hapo zamani, dhambi vipi jizuia?
Kwa mungu kaa tumboni, au kafara jitoa!!
Hayo si ya kitabuni, Musa alotuambia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

4.wokovu siyo imani, Bali dhambi kukimbia,
Pata okoka dhambini, bada mola mtambua,
Wokovu msalabani, ulaya wameshikia,
Vipi pombe vilabuni, zinaa nako kuua?
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

5.busara zitumieni, waungwana kutambua,
Pombe mzizi dhambini, si matusi si zinaa,
Duniani chunguzeni, wapi iliko zagaa,
Kama si msalabani, wapi palipozidia?
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

6.wokovu kweli ni nini!?, dhambini tao kutoa,
Mwenyezi Mungu yakini, kwa hoja kumtambua,
Kwa dalili akilini, kumuogopa jalia,
Na Upendo Wa moyoni, pekee kumpatia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

7.naswali kwa wanadini, vipi dhambi waingia,
Hali mnayo imani, ya Mungu wetu rabia!,
Hamumuogopi manani, duniani natulea,
Hamumpendi rabani, pepo alo iandaa,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

8.swali ninawajibuni, dhambi linaloibua,
Imani siyo yakini, ujinga pasi tambua,
Moyo ulo nayakini, dhambi haiwezi kaa,
Kama kutwa na gizani, pamoja wezi tulia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

9.mfano tuoneni, kwa ubongo kutambua,
Jiwe lile mkononi, tiba kila maradhia,
Chafwata nini wadhani, kifua takumbatia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

10.mfano tugeuzeni, huku tukifikiria,
Jiwe liwe mkononi, pasi wewe kutambua,
Kama lile mkononi, ni sumu yenye kuua,
Tabaki nalo wadhani, mbali utalirushia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

11.umepata somo gani, kama umefikiria,
Kwa asili insaani, vizuri twajivutia,
Vibaya vya hatarini, hatutaki karibia,
Sasa kwanini dhambini, hatutaki kujitoa?
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

12.enyi Ndugu wanadini, hakika yupo jalia,
Tafuta kweli yakini, dhambini hutojitia,
Utakuwa adhabuni, kila tendo kikosea,
Pakufikia Motoni, waovu wataingia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

13.akili zitumieni, yakini kuitambua,
Mifano ya duniani, michache kuangalia,
Hutobaki kiburini, hatari kikuingia,
Mifano ya hapa chini, kwa busara angalia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

14.je tautia motoni, mkono kifurahia?
Mlimani kileleni, chini tajiangushia?
Kwa hiyari kisimani, radhi utajitupia?
Kama si woga kwanini, hatari hutoingia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

15.je utalala relini, gari moshi La kujia?
Mkono tia kinywani, mwa simba alo na njaa,
Hautotoka chumbani, moto ukikuwakia,
Hutoruka kitandani, nyoka ukimlalia?
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

16.hatari za duniani, kwa woga utajitoa,
Vipi hatari mbinguni, kwanini wakurubia,
Umeikosa yakini, baya dhambi hujajua,
Heri kuwa mautini, si mola kumkosea,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

17.za juu juu imani, sababu kuangamia,
Adhabu ilo Motoni, wanadhani ni mzaa,
Wadhani wameamini, mola wajamtambua,
Qiyama hawaamini, mola hatotufufua,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

18.nimefika ukingoni, mwenye akili kajua,
Wokovu hasa ni nini, dhambi utakuokoa,
Mola ya kweli yakini, ndiyo Tiba maradhia,
Taokoka tambueni, peponi mtaingia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

Masihi Omary Kisagwa

NDOA

Twakushukuru Rabana, Ulopitisha harusi
Kwa utulivu mwanana, tena pasipo tatasi
Japomambo yamebana, Umeitia wepesi
Twakuomba Rahmani, ibariki ndoa hii.

Leo siku ya Harusi, sote tunashangilia
Tena bila wasiwasi, ndugu tunafurahia
Kwa baraka za Kudusi, Dua tunawaombea
Twakuomba Rahmani, ibariki ndoa hii.

Bibikani mwana wangu, Leo umesitirika
Ni binti wa kakangu, Ali Mbambwa msifika.
Umepata mkwe wangu, Kijana wa lako rika
Twakuomba Rahmani, ibariki ndoa hii.

Ukatulize akili, Ndoa sio masihara
Mumeo ukamjali, na ukawe mke bora
Uwe na njema kauli, hutacharazwa bakora
Twakuomba Rahmani, ibariki ndoa hii.

Mumeo ukamlee, mnapokua chumbani
Simkere kwa mayowe, ajihisi yu motoni
Kwa mahaba kamkoe, umdembe faraghani
Twakuomba Rahmani, ibariki ndoa hii.

Ewe Mwanangu kipenzi, wosia nakupatia
Ukufae kwenye Penzi, lisije kukukimbia
Sala ndo kubwa hirizi, usende kupuuzia
Twakuomba Rahmani, ibariki ndoa hii.

Mkwe wetu wa hidaya , mke tumekupatia
Shafii Bin Inaya, mwema kwenye jumuia
Dini siipige ngwala, mwisho mkaja jutia
Twakuomba Rahmani, ibariki ndoa hii.

Leo umekua tunda, katika wake mtima
Hanaye mwingine nyonda, twakujulisha mapema
Daima atakupenda, kwa jina lake Karima
Twakuomba Rahmani, ibariki ndoa hii.

Rabbi Ghafuru Mjenga, kizazi Awajalie
Kije dini kuijenga, haki kiipiganie
Dunia 'sije wazinga, wakanifanya nilie
Twakuomba Rahmani, ibariki ndoa hii.

Mwisho zangu shukurani, Namshukuru Rahima
Kanijalia hisani, nikaweza kuyasema
Pasipo kuoona soni, kinywani sikuguguma
Twakuomba Rahmani, ibariki ndoa hii.

Rajabu Abasi Mkieti
Al-Wattani _Mlezi
Masjid Ihsan- Tanga 15-OCT -2020

MWANA WA BARAKA

Rabi Ilahi Ghafuru, Jalilu Mola Rabuka
Wallahi nakushukuru, Shukurani kufurika
Kwa Mwana kunidhukuru, wakiume msifika
Uwe Mwana wa baraka, Mtoto wetu Raahil

Mtoto wetu Raahil, uwe Mwana wa baraka
Atakubariki Jalali, Baraka za kumiminika
Hilo naomba taamuli, mimi tena sinashaka
Uwe Mwana wa baraka, Mtoto wetu Raahil.

Mimi na mama Rehema,kheri tunakuombea
Malezi yalomema, sote tutakupatia
Ya dini yake Karima, Pamoya na ya dunia
Uwe Mwana wa baraka, Mtoto wetu Raahil

Mola akuhifadhi, katika hii dunia
Akukinge na maradhi, ili uweze kukua
Uje dini uikidhi, kwa heshima na Takua.
Uwe Mwana wa baraka, Mtoto wetu Raahil

Jamati yake raufu, uishike tena sana
Naye Masihi mtukufu, kwetu ndio sayidina
Khalifa wetu Ashirafu, Amir ul Muminina
Uwe Mwana wa baraka, Mtoto wetu Raahil.

Nusrati mke wangu, hongera tena hongera
Mama wa watoto wangu, kuzaa ni jambo bora
Pole kwa yote machungu, utaipata sitara
Uwe Mwana wa baraka, Mtoto wetu Raahil

Mimi babayo Rajabu, bado ningali kijana
Na Abasi ndio babu, katawafu mwaka jana
Muombea kwa Habibu, ghofira mola rabana
Uwe Mwana wa baraka, Mtoto wetu Raahil.

Wakatabahu kwaheri,uyashike nilosema
Ukidharau hatari, hapa mwisho na simama
Nakuombe mazuri, kwa mpaji Mola karima
Uwe Mwana wa baraka, Mtoto wetu Raahil.

Rajabu Abasi Mkieti
Al-Wattani -_Mlezi
Masjid Ihsan- Tanga

DAWA NENDA KWA MOLAO

Mambo yakikuelemea, usipoteze wakati
Kutwa kiguu na njia, kwa wale wasaka noti
Si waganga nakwambia, hoja yao sharubati
Dawa nenda kwa Molao, ufate tiba kamili

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)
Kiwalani, Migombani, Dar es salaam

Korongo na Nyoka



Msituni karibuni na mkondo wa ziwa paliishi korongo na mke wake. Walikuwa hawana furaha kabisa. Kila mara mke akitaga mayai kwenye kiota chao, nyoka kobra mweusi aliyeishi katika tundu mtini, huyala yote. Korongo alikuwa na rafiki yake kaa. Alikwenda kwa rafiki yake kaa na wakasimuliana majonzi. "najisikia kukosa matumaini... Yule mwizi mviziaji amekula mayai yetu tena," alilalama korongo kwa hasira.

"Usihofu," alisema kaa kwa faraja. "Usikose tumaini wakati unarafiki kama mimi. Tutapata ufumbuzi wa hili."

Kaa aliketi akitafakari mpango. Ghafla akaruka na kukimbilia kwa korongo.

"Rafiki, nina mpango mzuri," alisema kaa na akanong'oneza jambo sikioni kwa korongo.

Korongo akapaa kurejea kwenye kiota chake na kumwambia mkewe kuhusu mpango wote wa kaa. Alikuwa na furaha sana.

"Una hakika hili litafanikiwa?" aliuliza mke.

"Natumai hatufanyi makosa. Fikiri mara mbili kabla ya kuuendea mpango."

Lakini korongo alikuwa na hamu ya kuujaribu mpango. Korongo akapaa hadi mkondoni mwa ziwa na kuanza kuvua. Alipata samaki kadhaa wdogo na kwenda nao kwenye shimo alimokuwa akiishi nguchiro. Aliangusha samaki mmoja mlangoni. Kisha akaweka samaki mwingine mbali kidogo na yule wa mlangoni. Akirudia hivi, alitengeneza msururu wa samaki ukielea kwenye mti kilipo kiota chake.



Nguchiro aliipata harufu ya samaki na akatoka shimoni. "Ah, samakiii!" akashangazwa nguchiro kwa furaha na akamla. Kisha kafuatilia msururu wa samaki. Alipokaribia mti wanapoishi nyoka na korongo, msururu ukaishia. Asione samaki zaidi, akaangaza angaza.

Ghafla akakutana na nyoka kobra mweusi chini ya mti. Alipomuona nguchiro, nyoka akapambania maisha yake. Wote walipigana kwa muda mrefu na hatimaye nguchiro akamuua nyoka. Korongo waliokuwa wakitazama mpambano kutokea kwenye kiota chao wakatanafusi.

Siku iliyofuata nguchiro alianza kufuata msururu ule ule akitumainia kupata chakula zaidi. Alipofika kwenye mti msururu ukakoma, akaamua kupanda mtini kutafuta chakula.

Korongo waliokuwa wamekwenda ziwani walipokuwa wakirejea walikuta nguchiro akishuka mti. Walipotazama kiotani kwao, wakagundua safari hii, nguchiro alikula mayai yao yote.

"Yala! Tumemuondosha adui mmoja na kupata mwingine," alisema korongo akimwambia mkewe.

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno 24 hapo chini kwa kuyazungushia na Penseli

Amana	Tabia	Baba	Uadilifu
Kujikinga	Uongo	Kutoa	Urafiki
Subira	Anasa	Tamaa	Binadamu
Unyofu	Kusamehe	Upotofu	Maafa
Amani	Tadbiri	Biashara	Uadui
Kukosa	Upole	Kutosheka	Usawa

B	J	T	C	E	A		A	U	K	Y	D	G	L	R	
G	C	C	L	W	L	U	S	A	N	Y	G	D	A	A	R
N	M	O	A	A	D	M	O	D	L	K	V	R	G	X	N
L	P	S	I	D	N	A	K	U	Y	D	A	N	N	N	B
U	U	B	Z	T	A	D	U	I	N	H	I	U	P	F	N
A	A	L	P	N	N	A	K	B	S	K	B	F	C	X	P
T	N	B	A	B	A	N	M	A	I	W	U	I	I	T	J
M	U	A	N	Y	M	I	I	J	K	N	F	L	R	K	W
K	J	N	S	P	A	B	U	R	I	F	O	I	I	U	T
M	C	P	Y	A	K	K	M	L	F	K	T	D	B	S	A
K	A	N	B	O	Q	N	G	H	A	N	O	A	D	A	M
A	U	A	D	V	F	Y	C	T	R	F	P	U	A	M	A
M	R	T	F	H	T	U	R	H	U	W	U	Q	T	E	A
A	M	Z	O	A	K	U	T	O	S	H	E	K	A	H	R
N	N	M	Q	A	S	U	B	I	R	A	Y	C	P	E	R
I	N	Q	G	N	M	G	R	U	O	N	G	O	W	Q	T

UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



Tambi za nyama ya kusaga na uyoga

Na **Mtandao**



Mahitaji

500 g/ nusu kilo nyama ya kusaga
250g/ nusu paketi ya tambi
Kitunguu maji kimoja kikubwa
Nyanya 3 za wastani
Kijiko 1 cha chakula kitunguu saumu cha kusaga
Kijiko 1 cha chakula tangawizi ya kusaga
Nusu x3 hoho mchanganyiko zilizokatwakatwa
Vijiko 3 vya chakula mafuta ya kupikia
Vikombe 2 uyoga (ukipenda)
Karoti 1 kubwa
Vikopo viwili vya nyanya za kusaga (2 x 70 g)
Chumvi na pilipili manga kwa kuonja
Jibini ya chaguo lako ya kunyunyizia juu (ukipenda)
Majani ya kotimiri ya kunyunyizia kwa juu (ukipenda)

Maelekezo

Andaa viungo; katakata uyoga, karoti, pilipili hoho na kitunguu maji; twanga kitunguu saumu na tangawizi, weka pembeni
Saga nyanya kwenye mashine ya kusagia kupata rojo, weka pembeni
Kwenye sufuria katika moto wa wastani, chemsha mafuta. Ongeza kitunguu maji. Pika mpaka kilainike ila kisikauke
Ongeza kitunguu saumu na tangawizi. Pika kwa dakika kama 2; au mpaka harufu ya ubichi iishe
Ongeza nyama, chumvi na pilipili manga. Kaanga kiasi mpaka nyama ianze kupata rangi ya kahawia, kama dakika 5
Ongeza rojo ya nyanya. Koroga vizuri, funika na mfuniko. Acha nyama iive moto wa chini kwa dakika kama 15, au mpaka iive vizuri na maji yakaukie. Ikibidi ongeza maji kiasi
Ongeza uyoga na karoti kwa dakika kama 1 nyingine
Weka hoho, acha ziive kwa dakika 1 nyingine
Ongeza nyanya ya kopo na maji kiasi, pika kwa dakika chache; au mpaka mbogamboga ziive kama utakavyopenda. Ipua, weka pembeni
Chemsha spaghetti/ tambi kulinganya na maelekezo ya kwenye pakiti. Zikiiva, zichuje maji halafu zipake mafuta uchanganye vizuri ili zisishikane
Rudisha nyama kwenye moto. Ongeza Tambi kwenye mchanganyiko wa nyama na maji kidogo yakihitajika. Changanya vizuri
Pakua na jibini na majani ya kotimiri kama utapenda
Furahia.

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA^{AS}

Juu ya Qurán Tukufu

Hazrat Masih Mau' a.s anasema: Qurán Tukufu ni sanduku la johari, lakini ni wachache wanaofahamu ukweli huu.

(Malfudhat, Jalada 2, uk. 344)

DARASA LA QUR'AN TUKUFU

KUJITAKASA NI KATIKA NJIA YA RADHI YA ALLAH

Na **Musa Salum Mgeleka -** 0717 504 690

(ٱلَّذِى يُؤۡتِى مَالَهُۥ يَتَزَكَّىٰ)

Ambaye hutoa mali yake kujitakasa. Surah 92:19

UTAKASO ni njia ya kukifanya chema 2:130. Mwanadamu amezungukwa na Mali, vitu na watu. Maisha yake yote huhitajika kuwa Mema na ya Uchamungu mpaka vitu anavyotumia na vilivyomzunguka. Wakati fulani mwanadamu hufanya Jitihada za kuwa mwema kwa kutenda matendo mazuri na Mema. Jitihada hizo huwa hazitoshi kumfanya Mwema aliyekamilika ikiwa Mali na vitu anavyotumia na vinavyomzunguka vikiwa vimebeba vinasaba vya Uovu. Hii hutokana na Mali na vitu halali kukaa muda mrefu basi muda unavyopita Uhalali wa vitu hivyo hukosekana na kugeuka kuwa viovu na kuvitumia kwake Mwanadamu huanza Kumeza Uovu. Au Kukaa na Kutumia na vitu viovu huku akiwa Mwema basi hutafuna wema wake.

Mfano Mali halali iliyokaa Mwaka mzima mali hiyo sio halali tena kuitumia kabla ya kutoa Zaka. Kipato kilicho chumwa sio halali kabla ya Kujitolea Chandas ukiitumia bila kutoa basi utakuwa unakula Uovu na hatima yake kuwa Muovu. Tunatakiwa kujitolea Sadaka kwa ajili ya Ustawi wa watumishi wa Dini na Masikini na Ndugu na Wasafiri na Wenye matatizo kwa kila kipato chako halali na usipofanya hivyo utakuwa unauwa Moyo wako na Huruma kutoweka na hatima yake ni Uovu. Nafsi inapaswa kuendelea kusikia na kupata mawaidha mema kila wakati na kwa uchache kwa wiki mara moja ikaandaliwa kama siku ya Ijumaa na Mtu asipopata mawaidha kwa muda mrefu angalau wiki tatu nafsi yake inakufa.

Ili Mwanadamu Adumu kwenye Wema yampasa kwanza vitu vinavyomzunguka vyote na anvyotumia Vitakasike na ndipo aweze kuishi na Kukaa kwa wema. Wema wetu unaweza kuwa unaenda ukipungua na kupotea kwakuwa tunaishi na kukaa na vitu visivyo takasika. Na maana dhahiri ya Utakaso ni Mali. Mali inanunua kila kitu chako. Haupo Wema au Ibada yeyote ila Imeambatanishwa na Utakaso yaani Kujitolea Mali na Nafsi. Sala bila Utakaso haistawi wala Matendo Mema bila Utakaso ni Jitihada zinazopotea kwa Urahisi. Njia ya Utakaso ni katika Radhi ya Allah na Radhi ya Allah ni mlango wa Ufunguo wa kila kitu akiitajio Mwanadamu pamoja na Riziki.

.....hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda wanaotubu na wanaojitakasa. Surah 2:223

Mola wetu, Ututimizie nuru yetu, na Utughofirie; hakika Wewe ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu. Amin

MATUKIO KATIKA PICHA





Wataalamu wakirekebisha na kutengeneza mfumo wa sola na MTA kwa ajili ya wanajumuiya wa tawi la Kidanda, Shinyanga



Amir na Mbashiri Mkuu akiongoza uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa Msikiti katika eneo la Kazole karibu na Dares Salaam





Maonyesho ya vitabu Meya



Maonyesho ya vitabu Meya





Maonesho ya Qur'ani Tukufu na ya vitabu vingine vya dini mlangoni mwa Ukumbi wa Mkapa soko mtola, Mbeya Mjini



Sheikh wa Mkoa wa Dodoma wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya alishiriki katika kikao cha amani wilayani Dodoma na aliwapa waheshimiwa RPC na OCD Kitabu cha Khalifa Mtukufu (atba) kuhusiana na Amani



Sheikh wa mkoa wa Mbeya akiwapa zawadi ya vitabu viongozi wa Dini walioshiriki katika kwenye kongamano la amani mkoani Mbeya na maonesho ya vitabu

Ijazul Masih - Muujiza wa Masih Mau'ud



Sheikh Muzaffar Durrani
Rabwah, Pakistan

Seyidna Ahmadas Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya alizaliwa katika kijiji cha Qadian. Hakuwahi kusoma shule wala madrasa yoyote, isipokuwa katika utoto wake alifundishwa kidogo nyumbani masomo ya awali na baadhi ya walimu. Baadhi ya masheikh walidhani kwamba mtu ambaye alizaliwa katika kijiji cha India na kutopata fursa ya kuenda kusoma madarasani huwa hawezi kujua lugha ya Kiarabu.

Hivyo, wakati Seyidna Ahmadas alipodai kuwa yeye ni Masihi Mau'udi na Imamu Mahdi, wapinzani wakapiga makelele na kudai kwamba mtu ambaye hajui hata lugha ya Kiarabu, lugha ya sheria ya dini ya Kiislamu, atawezaje kufundisha na kuongoza Uislamu.

Seyidna Ahmadas kwa kweli, hapo kabla hakujua lugha ya Kiarabu kiasi cha kutosha. Kwa hiyo alimuomba Mwenyezi Mungu aliyemtuma kwamba apewe jibu la swali hili na afundishwe lugha ya Kiarabu. Na kweli ikatokea hivyo hivyo. Seyidna Ahmadas alitangaza kwamba Mwenyezi Mungu amemfundisha mizizi elfu arobaini (40,000) ya maneno ya asili ya lugha ya Kiarabu katika usiku mmoja tu. Hilo lilikuwa sio tu tangazo tupu, bali baada ya hapo Seyidna Ahmadas aliandika vitabu 25 katika lugha ya Kiarabu akieleza masomo ya dini. Sasa akawaita wapinzani hao waje washindane naye kwa ufasaha na ujuzi wa lugha ya Kiarabu.

Seyidna Ahmadas alileta maoni mazuri kwamba badala ya kushindana kwa njia nyingine, tushindane katika kuandika maelezo ya Kurani Tukufu katika lugha ya Kiarabu na tuyachapishe. Kwa njia hii itajulikana kwamba nani anajua lugha ya Kiarabu na nani anapiga makelele ya bure. Pia kwa kupatikana maelezo ya Kurani watu watafaidika nayo. Hapo masheikh wote wakanyamaza. Seyidna Ahmadas akawajulisha na kuwakumbusha mara kwa mara lakini wote wakakwepa.

Kisha Seyidna Ahmadas akawambia masheikh kwamba: Enyi masheikh wa India, mnaweza kujumuika na masheikh wa nchi za Misri, Shamu na Uarabuni. Kisha njooni nyote kwa pamoja tuandike maelezo ya Kurani. Wakati Seyidna Ahmadas alipoona kwamba bado hawapati ujasiri wa kukabiliana naye, basi akaamua kuwarahisishia kazi, ili wapate ujasiri wa kuingia katika mapambano ili ukweli wa mambo udhihirike. Hapo akawambia kwamba kama mnaona kutoa maelezo ya Kurani nzima ni jambo kubwa sana na gumu, basi tushindane kuandika tu maelezo ya sura moja tutakayoichagua kwa njia ya kura. Lakini hata hivyo hakuna Sheikh yeyote aliyejitokeza, ingawa hapo awali walijigamba sana na kupiga makelele.

Mwishowe Seyidna Ahmadas akatangaza kwamba mimi nimewakaribisheni sana katika mashindano haya, lakini hadi sasa sijapata jibu lolote kutoka kwa Sheikh yeyote yule. Sasa mimi mwenyewe nimeamua kuchagua Suratul Faatiha na kuyaandika maelezo yake kwa jina la Ijazul Masihi.

Kwa hiyo akaandika na kukichapisha kitabu hiki mnamo tarehe 20.02.1901 na aliwapelekea kitabu hicho wapinzani kwa njia ya posta rejista. Akatoa hata changamoto ya kumtaka mwanazuoni yeyote aandike mfano wa kitabu hiki.

Baada ya kupata bishara kutoka kwa Allah, Juu ya jalada la nje la Kitabu hicho akaandika hivi:

اِنَّهٗ كِتَابٌ لَيْسَ لَهٗ جَوَابٌ مَنْ قَامَ لِلْجَوَابِ وَ تَنَمَّرَ فَسَوْفَ يَرٰى اَنَّهٗ تَنَدَّمَ وَ تَذَمَّرَ ۔

Yaanihikinikitabukisichojibika. Mtu yeyote atakayesimama kukijibu na kujiandaa kufanya hivyo, bila shaka atajikuta akiwa ni mwenye majuto, aliyefedheheka na kuangamia.

Tena Seyidna Ahmadas alisema kwamba wanazuoni hawataweza kuleta mfano wake. Mwenyezi Mungu atazivunja kalamu zao na kuziharibu akili zao wasiweze kuandika mfano wa kitabu hiki (uk.37). Hata kama wajumuike na wasaidiane mababa zao, wana wao, wenzao, masheikh wao, wenye akili wao na mafakihi wao kuleta mfano wa maelezo ya Suratul Fatiha kama hayo ndani ya muda maalumu uliopangwa, hawataweza kamwe kuleta mfano wake, hata kama wasaidiane wao kwa wao. (uk.55)

Hakuna Sheikh yeyote aliyediriki kujitokeza kuleta mfano wa kitabu hicho kiitwacho Ijazul Masihi mbele ya Mjumbe na simba huyu wa Allah katika muda wake maalumu, wala katika uhai wa Seyidna Ahmadas wala katika miaka 120 iliyopita hadi leo.

Kama iulizwe kwamba je, kuandika kitabu ni muujiza, ilhali watu wanaandika vitabu kila siku? Basi jawabu lake ni kwamba kuandika kitabu si kitu lakini kuandika kitabu kwa njia ya mashindano, na kutangaza kabla kwamba Mwenyezi Mungu Amenipasha habari mapema kwamba hakuna mtu yeyote anipingaye atakayeweza kuandika kitabu cha aina hiyo na kisha kusisitiza kwamba kamwe hawataweza asilan kufanya hivyo na yeyote atakayejaribu na kudiriki kufanya hivyo, Mungu Ataivunja kalamu yake isiweze kudiriki kukubali changamoto hiyo na hatimaye itokee hivyo hivyo kwamba wapinzani wote washindwe kufanya hivyo, huo unakuwa tu ni muujiza uliothibitika kwa viwango vyote, hata kama makafiri watake au wasitake.

Twajua kuwa Mtume Mtukufu Muhammadsaw alipewa Kurani Tukufu ambayo kwa dhahiri ni kitabu tu, lakini Mwenyezi Mungu Aliwatupia wapinzani tambio kwamba:

وَ اِنْ كُنْتُمْ فِيْ رَيْبٍ مِّمَّا نَزَّلْنَا عَلٰى عَبْدِنَا فَاْتُوْا بِسُوْرَةٍ مِّنْ مِّثْلِهٖ وَادْعُوْا شُهَدَآءَكُمْ مِّنْ دُوْنِ اللّٰهِ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ۝

Na ikiwa mna shaka kwa hayo Tuliyomteremshia Mtumishi wetu, basi leteni sura iliyo mfano wa hii, na muwaite wasaidizi wenu ghairi ya Mwenyezi Mungu ikiwa mnasema kweli. (Al-Baqara, 2:24)

Pia Alisema kwamba:

قُلْ لَّئِنِ اجْتَمَعَتِ الْاِنْسُ وَ الْجِنُّ عَلٰٓى اَنْ يَّاْتُوْا بِمِثْلِ هٰذَا الْقُرْاٰنِ لَا يَاْتُوْنَ بِمِثْلِهٖ وَ لَوْ كَانَ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ ظَهِيْرًا

Sema: Kama wajikusanye watu na majinni kwa kuleta mfano wa Kurani hii, hawataweza kuleta mfano wake hata kama wasaidiane wao kwa wao. (Banii Israaiil, 17:89)

Yaani Mtume Mtukufu Muhammadsaw alipewa Kitabu cha Kurani Tukufu. Wengine wote waliambiwa kuleta mfano wake lakini walishindwa kufanya hivyo. Kwa njia hii Kurani imekuwa ni muujiza mkubwa wa Mtume Muhammadsaw.

Vile vile Seyidna Ahmadas alipewa muujiza wa kutoa maelezo ya kina ya Kurani Tukufu. Akaeleza na kuandika maelezo ya Suratul Fatiha lakini wengine wote walishindwa kuleta mfano wa aina hiyo. Na ndio sababu akakiita Kitabu hicho kwa jina la Ijazul Masihi yaani Muujiza wa Masihi Mau'udi.

Waheshimiwa wasomaji, Wakati makafiri walipoitwa kuleta mfano wa Kurani Tukufu, wakajigamba hivi:

وَاِذَا تُتْلٰى عَلَيْهِمْ اٰيَاتُنَا قَالُوْا قَدْ سَمِعْنَا لَوْ نَشَآءُ لَقُلْنَا مِثْلَ هٰذَآ اِنْ هٰذَآ اِلَّآ اَسَاطِيْرُ الْاَوَّلِيْنَ ۝

Yaani wanaposomewa Aya zetu, husema: Tumekwishasikia. Tungetaka bila shaka tungesema kama haya. Haya si chochote ila ni hadithi tu za watu wa kale. (Al-Anfaal, 8:32)

Hivyo ndivyo wapinzani wa Seyidna Ahmadas tangu miaka 120 wanatapatapa tu kwamba 'Ijazul Masihi' si chochote, waweza tu kuandika mfano wake. Vile vile wanakosoa kosoa tu na wakifuata nyayo za makafiri wanatuhumu kuibia maneno ya vitabu vya zamani. Lakini ukweli ni huu kwamba wapinzani wote wa zama zote wa Seyidna Ahmadas wameshindwa vibaya sana kuleta mfano wa Ijazul Masihi. Huo ni msaada mkubwa kwetu na pigo kubwa kwa wapinzani kutoka kwa Allah sub'hanahu wa ta'alaa. Mwenye macho, na aone. Mwenye masikio, na asikie.

اِسْمَعُوا صَوْتَ السَّمَآءِ جَآءَ الْمَسِيْحُ جَآءَ الْمَسِيْحُ

Ndugu zangu wapendwa, Isikilizeni sauti ya mbingu kwamba Masihi ameshafika, Masihi Mau'udi ameshafika.

Sh. Durrani.

Kwa nini Biblia Ni Jibu Wanamkana Nabii Issa kuwa Si Yesu?

Kutoka uk. 4

Simoni alie mwita jina la Petro na Adrea nduguye na Yakobo na Yohana na filipo na Baritamoyo na Matayo na Tomaso na Yakobo wa Alipayo na Simoni alie itwa Zelote na Yuda wa Yakobo na Yuda Iskariyote . ndie alikuwa msaliti

Je haujaona tofauti katika majina pia ya wanafunzi wao? Hapa wapo Mayuda wawili . Mmoja muungwana na mwingine msaliti

Je kwa Yesu mkimbizi alikuwa na Myuda ao wawili ? je mbona hapo hawakutoa hukumu ya kumkataa Yesu mmoja dhidi ya Yesu mwingine ?

Nadhani kama kundi hilo halifanyi propaganda wangekuwa watafiti wa maandiko na uchunguzi wa hoja wange ikataa bibilia kwa ujumla na sio Quran .

Tena wanadai kushangaa eti pindi Waislam walipo fanya maandamano yakupinga Uungu wa Yesu eti hawakuona bango lililo andikwa Issa si Mungu .Sasa sijui hao waandishi wa biblia ni jibu walitaka waone bango lisilo na madai na dhani wao ndio wana dai kuwa Yesu ni Mungu ,Hivyo kama wanata ka waislam wa seme Issa siyo Mungu inatakiwa simba ulango au Daniel waseme Issa ni Mungu hiyo ndio kauli wanayo taka wataisikia mfano wao wamesema Issa siyo Yes una waislam tuna sema Issa ndie Yesu ndio kusema kwamba kazi waislamsio kusema sema kazi ya waislam sio kusema sema kazi ya waislam ni kujibu hoja za Biblia sura 5:117:Na mwenyezi Mungu atakapo sema ewe Issa bin Mariam je wee uliwaambia watu nishikeni mimi na mama yangu kuwa Waungu wawili baada ya Mwenyezi Mungu ? Atasema wewe ndie mtakatifu haini pasi kusema ambayo sina haki (ya kujisema) kama ningeli sema bila shaka ungelijua unayajua yaliyomo nafsini mwako hakika wewe ndie ujuwaye saana mambo ya ghaibu .

Hoja hiyo iliyo jibiwa na Quran ndio inayo fanya biblia nijibu wamkatae Issa, maana kumkubali ni kuukataa uungu wa Yesu wanaemtangaza kama mungu.

HOJA YA PILI

Itaendelea toleo lijalo

Watu Walio Bora Kabisa: Masahaba wa Badr

Kutoka uk.12

Yemen, Mtume Mtukufu (saw) alimshauri mambo kumi, moja wapo likiwa ni kujiepusha na ubadhirifu. Alimshauri pia ashughulike na watu wa Yemen kwa upole na tabia nzuri.

Khalifa Mtukufu (aba) anasema hapa Mtume Mtukufu (saw) anawafundisha Waislamu kuishi na watu wengine kwa tabia nzuri. Lakini je! Wao wanafuata mafundisho haya leo? Ingawa leo hii Waislamu ulimwenguni kote wanasherehekea siku ya kuzaliwa kwa Mtume (saw).

Kujitolea kwa Hazrat Mu'aaz (ra)

Khalifa Mtukufu (aba) anasema safari moja, Hazrat Umar (ra) alimtuma mtu kwa Hazrat Abu Ubaidah bin al-Jarrah (ra) na dinari 400 na akamwambia ampe pesa hizi naye aone atazitumia vipi. Alipompa pesa Hazrat Abu Ubaidah (ra), alimwita mmoja wa wafanyakazi wake na kumuamuru asambaze fedha hizi kwa kaya mbalimbali zinazohitaji pesa hizi. Halafu Hazrat Umar (ra) akatuma kiasi hicho cha pesa kwa Hazrat Mu'aaz (ra) na tena akaamuru kwamba mtu anayewasilisha abaki palepale ili kuona jinsi anavyozitumia. Wakati Hazrat Mu'aaz (ra) alipopokea pesa, yeye pia aliagiza kwamba pesa hizo zigawanywe kwa kaya mbalimbali zinazohitaji. Kwa wakati huo, mke wa Hazrat Mu'aaz (ra) alisema kwamba wao pia ni masikini sana na wanahitaji pesa kwani hawakuwa na chochote. Mpaka wakati ule, Hazrat Mu'aaz (ra) alikuwa tayari amesambaza pesa na alikuwa amebakisha dinari mbili tu, ambazo alimpa mkewe. Hazrat Umar (ra) aliposikia habari hii, akafurahi sana.

Khalifa Mtukufu (aba) anasema, tukio hili, na haswa yale maoni yaliyotolewa na mke wa Hazrat Mu'aaz (ra) yanaonyesha kwamba Hazrat Mu'aaz (ra) hakutumia pesa alizopokea kuishi kifahari na maisha ya starehe.

Kufariki kwa Hazrat Mu'aaz (ra)

Khalifa Mtukufu (aba) alisoma tukio la kufariki kwa Hazrat Mu'aaz (ra). Hazrat Mu'aaz (ra) alikuwa amelala kitandani wakati alipokuwa anasimulia habari aliyokuwa ameambiwa na Mtume (saw), nayo ni: "Kila mtu atakayekiri kuwa Mwenyezi Mungu ni Mmoja na Muhammad (saw) ni Mtume Wake, ataingia peponi. Naye akasema (ra) habari hii hajawahi kumuambia mtu yeyote hadi leo kwa hofu kuwa watu wangetegemea jambo hili na kuacha kufanya mambo mengine muhimu. Sawa na masimulizi mengine, Hazrat Mu'aaz (ra) alikuwa analia katika nyakati zake za mwisho. Akasema hakuwa analia kwa sababu ya kuogopa kifo, bali alikuwa analia kwa sababu kulikuwa na vikundi viwili, lile linaloenda peponi na lile jingine linaloenda motoni, na hakujua atakuwa katika kundi gani.

Hazrat Abdullah bin 'Amr (ra)

Khalifa Mtukufu (aba) anasema, sahaba wa pili ambaye angeangazia maisha yake ni Hazrat Abdullah bin 'Amr (ra).

Hazrat Abdullah bin 'Amr (ra) alitokana na tawi la Banu Salamah la kabila la Khazraj. Baba yake ni 'Amr bin Haram na mama yake ni Rubab binti Qais. Yeye ni baba wa Hazrat Jabir bin Abdillah (ra) na kwa hivyo alijulikana pia kama Abu Jabir. Alikubali Uislamu katika tukio la Baiati ya Pili huko Aqabah. Alishiriki katika vita vya Badr na aliuawa na kuwa shahidi wakati wa vita vya Uhud.

Mapenzi yake kwa Mtume Mtukufu (saw)

Khalifa Mtukufu (aba) alisoma simulizi kuhusu dada wa Hazrat Abdullah bin 'Amr (ra), ambaye baba yake, kaka yake, mume na mtoto wake wote waliuawa na kuwa mashahidi katika Vita vya Uhud. Yule dada alipopata taarifa ya mauaji yao, alikuwa na wasiwasi zaidi juu ya usalama na ustawi wa Mtume Mtukufu (saw). Alipojua kuwa Mtume Mtukufu (saw) yuko salama, akasema kuwa hajali kuuawa kwa mtu mwingine yeyote, maadamu Mtume Mtukufu (saw) alikuwa salama.

Khalifa Mtukufu (aba) alisoma simulizi nyingine kutoka kwa Hazrat Jabir bin Abdullah (ra) kwamba kabla ya kuondoka kwa Hazrat Abdullah bin Amr (ra) kwenda kwenye Vita vya Uhud, alimshauri mtoto wake kulipa madeni yake na kuwatunza dada zake. Asubuhi iliyofuata, Hazrat Abdullah bin 'Amr (ra) alikuwa wa kwanza kuuawa na kuwa shahidi. Mazishi yake yaliongozwa na Mtume Mtukufu (saw).

Khalifa Mtukufu (aba) anasema, ataendelea kumzungumzia Hazrat Abdullah bin 'Amr (ra) katika hotuba ya Ijumaa ijayo. In Shaa Allah.

TANGAZO LA IJTIMAA YA MAJLIS ANSARULLAH AHMADIYYA TANZANIA

Tanzim ya Ansarullah Ahmadiyya Tanzania inapenda kuwataarifu Ansarullah wote nchini kuwa Ijtimaa yao itakuwa tarehe 11-13 Disemba 2020, Kitonga, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam. In-Shaa-Allah.

Wote wanaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Limetolewa na Majlis Ansarullah Ahmadiyya Tanzania

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

SAFAR - RAB. I 1442 AH | OKT-NOV 2020 | TABOOK 1399 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu[saw]

"Mtume[saw] alikuwa anasema, "Pengine unalazimika kutoa sadaka, lakini hutoi, basi haramu inaangamiza mali yako ya halali. Bila shaka haramu haichanganyiki na halali ila inaihilikisha." (**Kashf-ul-Gumah**)

Watu Walio Bora Kabisa: Masahaba wa Badr

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 30/10/2020 iliyotolewa Masjid Mubarak, Islamabad, UK; baada ya Tashahhud, Ta'awwudh na Surat Faatihah, Khalifa Mtukufu, Hadhrat Amir ul Mu'miniin, Mirza Masroor Ahmad[atba] ('Ayyadahullahu Ta'ala Bi-Nasrihil Aziiz') alisema;



Masjid Mubarak: Hadhrat Khalifatul Masih V[atba] huhutubia Ijumaa kwa waaminio tokea na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

Ukarimu wa Hazrat Mu'aaz bin Jabal (ra):

Khalifa Mtukufu (aba) anasema kwa sababu ya ukarimu wake, kwa muda fulani alipata deni kubwa. Wale waliokuwa wanamdai walikwenda kwa Mtume Mtukufu (saw) kumwarifu kuhusu habari hii. Mtume Mtukufu (saw) alimuita Hazrat Mu'aaz (ra) naye akajua kuwa deni alilolipata lilizidi kiasi cha fedha alichokuwa nacho. Kwa hivyo, Mtume Mtukufu (saw) akasema yeyote atakayesamehe deni la Hazrat Mu'aaz (ra) Mwenyezi Mungu atamshushia rehema. Kwa hivyo watu wengi wakasamehe deni la Hazrat Mu'aaz (ra). Hata hivyo walikuwepo wengine waliobaki waliotaka deni lao lilipwe. Hazrat Mu'aaz (ra) akawalipa kiasi alichokuwa nacho kutokana na mali zake, lakini hata hivyo pamoja na kutoa kiasi kile deni lote halikuweza kumalizika, Mtume Mtukufu (saw) akaagiza apewe muda ili aweze kumaliza baadae.

Uaminifu wa Hazrat Mu'aaz (ra)

Baadaye, Mtume Mtukufu (saw) alimtuma Hazrat Mu'aaz (ra) kwenda Yemen kama Amir na alikuwa mmoja wa masahaba watano waliopewa dhamana ya kusimamia mambo ya Yemen. Kabla ya kuondoka kwake, Mtume Mtukufu (saw) alimwambia, kwa kuwa bado alikuwa na deni kubwa, ikiwa mtu yeyote atampa zawadi basi aipokee. Kwa ruhusa hii, Hazrat Mu'aaz aliweza kulipa deni lake kamili.

Khalifa Mtukufu (aba) anasema inasimuliwa na Hazrat Mu'aaz (ra) kuwa wakati anaondoka kwenda Yemen, Mtume Mtukufu (saw) alimsindikiza akitembea naye sambamba huku akimuambia huenda utakaporudi usinikute, ukapita tu kwenye kaburi langu. Baada ya kusikia haya, Hazrat Mu'aaz (ra) alianza kulia.

Nasaha ya Mtume Mtukufu (saw) kwa Hazrat Mu'aaz (ra)

Khalifa Mtukufu (aba) anasema inasimuliwa na Hazrat Mu'aaz (ra) kwamba wakati wa kuondoka kwenda

Endelea uk 11

KITABU

Toeni Fatwa

Kitabu hiki, kilichoandikwa na Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad Qadiani[as], Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi na mwanzilishi wa Jumuiya ya Ahmadiyya katika Islam, anatoa mwanga kwenye hali zisizo za kawaida zilizopelekea kutimia kwa bishara yake kuhusiana na kifo cha kiongozi wa Aryah Samaj, Pandit Lekhram, ambaye alikuwa maarufu kwa matusi dhidi ya Mtume wa Islam na dini yake. Katika kitabu hiki kidogo lakini kipana, mwandishi amejadili kwa ukamilifu kwamba Lekhram aliuliwa kwa matokeo ya ufunuo wa kitume aliokwishaupokea toka kwa Mola wake, na ambao umetimilizwa kama dhihirisho maalum la nguvu za kiungu.

Mwandishi pia amethibitisha, kwa hoja bainishi, kwamba mauaji ya Lekhram hayakuwa matokeo ya njama yoyote iliyopangwa na upande wa mwandishi, bali ilikuwa ni tukio lililotuka kwa mpatano hasa na ubashiri ulioletwa na mwanga wa funuo ya kiungu na neno la adhimu la Mungu.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com